BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuanza Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na kuweza kukutana katika Baraza lako tukufu kuendelea na majukumu yetu. Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kupitia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilipata fursa ya kupokea maoni kutoka kwa wadau mbali mbali pamoja na wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 93(4). Hivyo, Kamati inawashukuru kwa dhati wenyeviti na wadau wote kwa michango mbali mbali waliyoileta mbele ya Kamati ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia katika kufanikisha uandishi wa Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa kupitia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilikutana na Mawaziri na watendaji wa wizara, idara na taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Hivyo, kwa dhati kabisa Kamati inawashukuru wote waliohudhuria

hususan Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mipango Mhe. Jamal Kassim Ali kwa kushiriki katika vikao hivyo na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizoibuliwa wakati wa mjadala na hatimae Kamati kuweza kufanikisha kazi yake kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia marekebisho madogo uliyoyafanya ya wajumbe wa Kamati za kudumu za Baraza, kwa sasa Kamati ya Bajeti ina Wajumbe saba, na makatibu wanne. Naomba uniruhusu kuwashukuru kwa kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Anna Athanas Paul | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Harusi Said Suleiman | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Abdalla Ali Shauri | Katibu |
| 9. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 10. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 11. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| 12. | Ndg. Yustina E. Joseph | Msaidizi wa mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2020

### Ukuaji wa Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Ukuaji wa Uchumi wa nchi hutegemea hali ilivyo duniani kwa ujumla wake na kwa kulinganisha na mataifa mengine. Takwimu za kasi ya ukuaji wa uchumi Zanzibar katika mwaka 2020 zinaonyesha umefikia wastani wa asilimia 1.3 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2019 ambapo kasi hiyo inaridhisha ukilinganisha na nchi nyengine duniani. Aidha, kwa mwaka 2020 ukuaji wa uchumi unaridhisha kwa kuwa kuna baadhi ya sekta zimefanya vizuri ikiwemo sekta ya ujenzi na sekta ya uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya mwaka 2021/2022 ni bajeti ya mwanzo ambayo inaanza kutekeleza Dira mpya ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 yenye lengo la kuifikisha Zanzibar katika kiwango cha Juu cha Uchumi wa Kati (Higher Middle Income). Kwa kuzingatia mwelekeo wa hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2021, Kamati inaishauri Serikali kuandaa na kusimamia mazingira mazuri kwa ajili ya kuzinyanyua sekta nyengine zikiwemo kilimo na uvuvi pamoja na kuimarisha uwekezaji katika rasilimali watu ili kusaidia katika upatikanaji wa huduma bora za kijamii zikiwemo huduma za afya na elimu ambazo zinagusa wananchi moja kwa moja.

### Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Pato Halisi laTaifa kwa mwaka 2020 lilifikia thamani ya TZS 3,116 bilioni mwaka 2020 ukilinganisha na thamani ya TZS 3,078 bilioni mwaka 2019. Licha ya kuongezeka kwa pato hilo, kipato cha mwananchi mmoja mmoja kwa mwaka 2020 kimepungua na kimefikia TZS 2.53 milioni mwaka 2020 kutoka TZS 2.55 milioni mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu za kupungua kwa Pato la Mwananchi mmoja mmoja ni kukua kwa uchumi kwa kasi ndogo pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu. Kamati inaishauri Serikali katika Bajeti ya 2021/2022, kuhakikisha inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo itasaidia katika kupunguza wingi wa jamii iliyotegemezi kwa kuwapa fursa za ajira wananchi na kuongeza kipato kitakachowasaidia katika kukidhi mahitaji yao mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kukua kwa kasi kwa idadi ya watu kunapaswa kuende sambamba na kasi na uwezo wa Serikali katika kuwapatia wananchi wake huduma za msingi za kijamii ikiwemo elimu, afya na maji, kutoa fursa za mikopo ya biashara na ajira sambamba na kuwa na mipango mizuri ya matumizi ya ardhi, hususan kwa nchi za visiwa kama Zanzibar ambazo zina changamoto ya uchache wa rasilimali hiyo. Idadi kubwa ya watu inaweza kuwa na faida kiuchumi iwapo tutaitayarisha jamii ya uzalishaji badala ya kuwa na jamii ambayo wengi wanawategemea wachache.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ulilenga kutekeleza programu na miradi 94, ambapo jumla ya TZS 609.99 bilioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mpango huo. Kwa upande wa Serikali ilipanga kuchangia TZS 197.3 bilioni sawa na asilimia 32.3 ya bajeti ya maendeleo kutoka fedha za ndani na TZS 412.7 bilioni sawa na asilimia 67.6 zimepangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya TZS 166.3 bilioni zilitumika ikiwa TZS 49.2 bilioni sawa na asilimia 25 zilitoka Serikalini na TZS 117.1 bilioni sawa na asilimia 28 zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu hizi zinaonesha upatikanaji wa fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Serikalini na kwa Washirika wa Maendeleo ni mdogo sana na utekelezaji wa baadhi ya Miradi katika Wizara na taasisi za Serikali upo katika hatua za chini kabisa. Kamati inapata wasi wasi juu ya utekelezaji huo hasa ikizingatiwa kuwa utekelezaji wa miradi ni muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi. Hivyo, Kamati inashauri licha ya kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa fedha, watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia miradi kutekeleza vyema majukumu yao kwa kuhakikisha fedha inayopatikana inatumika kwa mujibu wa malengo na kwa ufanisi wa hali ya juu.

**UTEKELEZAJI WA MAENEO YA VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 HADI MACHI 2021**

**Mheshimiwa Spika,** Maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya 2020/2021 ni maeneo kumi na tatu (13). Katika utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, vipaumbele kumi (10) ndio vilivyoanza hatua za utekelezaji na vipaumbele vitatu bado havijaanza kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika vipaumbele vilivyokuwa havijaanza kutekelezwa ni pamoja na kipaumbele cha kuhuisha uchumi baada ya athari ya maradhi ya Korona kwa kutekeleza Mpango wa Kuhuisha Uchumi (Economic Recovery Plan – ERP) na kipaumbele cha kuimarisha uchumi wa buluu kwa kuandaa Mpango wa Matumizi ya Bahari na maeneo yake. Kamati inaitaka Afisi ya Rais Fedha na Mipango, kuzingatia utekelezaji wa vipaumbele vilivyoachwa katika bajeti ya 2020/2021 kwani baadhi ya vipaumbele hivyo vimeanishwa tena katika bajeti ya 2021/2022 . Aidha, Kamati inashauri kipaumbele cha kuhuisha uchumi baada ya

athari ya maradhi ya Korona kuangaliwa upya kwani janga la mardhi ya Korona bado ni tishio katika nchi mbali mbali duniani.

## UTEKELEZAJI HALISI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 HADI MACHI 2021

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mambo mengine, makadirio ya mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata huzingatia pia utekelezaji halisi wa makusanyo ya mapato kwa miaka iliyopita, ikijumuisha vyanzo mbali mbali vya mapato kutoka ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 1,579.2 bilioni katika mwaka wa fedha 2020/2021. Hali halisi ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kipindi hicho ni jumla ya TZS 723.3 bilioni sawa na asilimia 61 ya lengo la TZS 1,185.1 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa upatikanaji wa mapato kwa kipindi cha miezi tisa umefikia asilimia 61 tu ya lengo lililopangwa, na kwa kuzingatia kuwa bajeti inayoleta tija kwa wananchi inategemea sana upatikanaji mzuri wa mapato ya ndani na ya nje, Kamati inaishauri Serikali, kuendelea na usimamizi madhubuti wa taasisi zote zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato ili mapato yaweze kupatikana kama yalivyokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mripuko wa Maradhi ya COVID 19 ambao umeleta mtikisiko wa kiuchumi katika mataifa mbalimbali duniani na kuleta athari katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje. Katika Bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2020/2021, Serikali iliamua kuchukua hatua mbalimbali za kurekebisha sheria za kodi ili kuwapa unafuu wafanyabiashara, kuimarisha

ukusanyaji wa mapato na kumsaidia mwananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa marekebisho ya sheria yaliyofanyika ni kupunguza kodi ya ongezeko la thamani VAT kutoka asilimia 18% hadi 15% na kufuta kodi ya VAT kwa uingizaji wa vifaa vya uvuvi ili kuimarisha sekta ya uvuvi ambayo ina mchango mkubwa katika kuongeza pato la ndani. Aidha, kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam.12 ya Mwaka 2016 kwa kufuta tozo na ada mbalimbali zinazokusanywa na Serikali za Mitaa, Kufanya marekebisho ya Sheria za Kodi ya Majengo, Sheria Nam. 14 ya mwaka 2008, kwa kuongeza kifungu 7A (1) & (2) kinachompa nguvu Waziri mwenye dhamana ya fedha kuanisha Jengo au aina ya majengo yanayopaswa kulipiwa kiwango maalumu cha kodi ya majengo ili majengo hayo yaweze kukusanywa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwajali wananchi wake kwa kufanya uamuzi mzuri wa kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali kwa lengo la kupunguza kodi kwa wafanyabiashara mbalimbali na wajasiriamali wadogo wadogo. Kamati inaishauri Serikali inapopunguza viwango vya kodi kufanya ufuatiliaji ili kubaini iwapo marekebisho hayo ya Sheria ya kodi yanawanufaisha wananchi kwa kupata bidhaa na huduma nafuu badala ya kuwanufaisha wafanyabiashara pekee.

**Mheshimiwa Spika,** Katika marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam.12 ya mwaka 2016 ambayo imefuta Tozo na Ada mbalimbali za Serikali za Mitaa Kamati imebaini kutoshirikishwa ipasavyo Serikali za Mitaa katika marekibisho hayo, hali inayopelekea taasisi kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa kupangiwa viwango vidogo sana vya ada za leseni na taka kwa wafanyabiashara wakubwa wa maduka na hoteli za kitalii, hali

inayopelekea kutomudu gharama za uendeshaji wa mamlaka hizo kwa kufanya usafi wa miji pamoja na kushindwa kuanzisha miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali wakati wa kufanya marekebisho mbali mbali ya sheria za usimamizi wa fedha na kodi ni muhimu sana kuwashirika wadau pamoja na walengwa wa sheria hizo ili kupokea maoni mbalimbali yatakayoleta maelewano na kuondoa malalamiko. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua zaidi za kuimarisha ukusanyaji wa kodi kwa ufanisi ili kuzidhibiti mianya ya upotevu wa mapato na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa vyanzo vipya vya mapato.

**Matarajio ya Mapato Julai - Juni 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai - Juni 2020/2021 Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 1,024.9 bilioni sawa na asilimia 64.9 ya makadirio ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya jitihada mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali bado hali ya ukusanyaji wa mapato hairidhishi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali, wakati wa kuandaa bajeti kufanya uchambuzi wa kina wa makisio ya mapato na uwezo wa vyanzo vya mapato kwa kuzingatia hali ya mwelekeo wa uchumi kulingana na mazingira ya ndani na nje ya nchi.Kamati inasisitiza jambo hili, kutokana na ukweli kwamba pamoja na kuwa hali ya ukusanyaji mapato imeathiriwa na uwepo wa athari za maradhi ya Korona, wakati makisio hayo yalipopangwa tayari ilikwishajulikana kuwa hali ya uchumi haitokuwa ya kawaida na bado makisio yakawekwa makubwa sana.

## MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### Utekelezaji Halisi wa Matumizi Julai 2020 hadi Machi 2021

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya TZS 723.4 bilioni sawa na asilimia 62 ya makisio ya TZS 1,167 bilioni ya lengo la kipindi hicho yalitumika katika kipindi cha Julai-Machi 2020/2021. Kati ya matumizi hayo, TZS 550.1 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 72 ya makisio ya TZS 763.7 bilioni na TZS 173.2 bilioni zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 42.9 ya makisio ya TZS 403.3 bilioni. Aidha, hadi kufikia Juni 2021 Serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 1,024.9 bilioni sawa na asilimia 64.9 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 1,579.2 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini asilimia kubwa ya matumizi ya Serikali yametumika katika kazi za kawaida kuliko kazi za maendeleo. Hali hii ndio ambayo husababisha utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo kusuasua kutokana na ukosefu wa fedha ambazo kwa kiasi kikubwa ni mikopo na ruzuku kutoka kwa wafadhili na washirika wa maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusimamia taasisi zake za ukusanyaji wa mapato ili kuimarisha mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa bajeti kwa washirika wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati inaishauri Serikali kuzisimamia taasisi zake kwa kufanya matumizi yanayozingatia mipango kazi yao sambamba na kuzimamia taasisi hizo kwa ukaribu zaidi katika kutekeleza shughuli zote za manunuzi zinazofanyika ili kuhakikisha kuwa taratibu zinafuatwa na kupatikana kwa thamani ya fedha halisi zinazotumika.

### Mfuko wa Miundombinu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipopitia matumizi ya Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha miezi tisa Julai – Machi, 2020/2021, ilibaini jumla ya TZS

44.2 bilioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi kumi na tano (15) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo kiasi cha TZS 14.1 bilioni zimetumika katika kugharamia miradi minane (8) kati ya miradi kumi na tano (15) iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na asilimia 32 ya makadirio ya mwaka. Miongoni mwa miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa fedha za mfuko huo ni pamoja na ***Mradi wa Ununuzi wa Vifaa vya Zimamoto na Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Ushoni.***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapata wasi wasi juu ya utekelezaji wa miradi inayotumia fedha zinazotokana na Mfuko wa Miundombinu iwapo miradi hiyo ndio iliyolengwa kwa mujibu wa uanzishwaji wa mfuko huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia vyanzo vya mapato ya mfuko huo, ni vyema fedha zake zikatumika zaidi kwa ajili ya miundombinu ya msingi kama sheria ya mfuko huo ilivyoelekeza zikiwemo barabara za ndani ambazo bado ni eneo lenye changamoto kubwa, badala ya fedha hizo kutumika katika miradi ya kawaida. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu madhubuti wa utumiaji wa fedha zinazotokana na Mfuko wa Miundombinu ili kuepusha matumizi tofauti na malengo ya uanzishwaji wa mfuko huo.

**Deni la Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali ya Mapitio ya Hali ya Uchumi 2020 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2020/2021 inaonyesha hadi Machi 2021, Deni la Taifa lilifikia TZS 894.6 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 9.5 ikilinganishwa na deni la la TZS 816.6 bilioni liloripotiwa Machi mwaka 2020 .

**Mheshimiwa Spika,** Kiwango cha deni kilichoripotiwa kwa kipindi cha Julai – Machi, 2020/2021 kinaashiria kuwa deni letu bado ni himilivu ukilinganisha na Pato la Taifa. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali iangalie vigezo vyengine vya

kupima uhimilivu wa deni la taifa, kama vile kigezo cha uwiano wa deni na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi (Debt to Export) na uwiano deni na ukusanyaji wa mapato (Debt to Revenue). Vigezo hivi vitatupa vile vile njia bora ya kuweka mikakati ya kusimamia deni letu la ndani kwa umakini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali inapohitaji kukopa, kuchukua Mikopo yenye masharti nafuu na yenye tija kwa nchi yetu. Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo huweka masharti magumu yanayokwaza utekelezaji. Hali hii imejitokeza katika mradi wa miundombinu ya umwagiliaji maji unaotekelezwa kupitia mkopo wa Exim – Korea, ambao umelazimisha mshauri elekezi na mkandarasi atoke nchini kwao licha ya kuwa uwezo wao ni mdogo katika kutekeleza mradi huo.

**MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2021**

**Mheshimiwa Spika,** Kulingana na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2021, Pato la Taifa linatarajiwa kukuwa kwa kasi ya wastani wa asilimia 5.0 hadi 7.1 na ukuaji wa uchumi unatarajiwa kukuwa kwa kasi ya chini ya asilimia 5.2.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na mipango ya kuimarisha ukuwaji wa uchumi kila mwaka lakini bado Serikali haijaweka mikakati ya kuhakikisha kwamba, ukuwaji wa uchumi unakwenda sambamba hali halisi na maisha ya wananchi. Ni ngumu kueleweka kwamba uchumi umekuwa wakati hali za maisha za wananchi na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii bado ni duni.

**Mheshimiwa Spika,** Ili tuweze kufanikiwa kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wetu, Serikali haina budi kuimarisha upatikanaji wa

huduma za afya, maji, elimu na kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara. Kuharakisha ukuaji wa uchumi mpana na jumuishi wenye kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa na kunufaisha wananchi wengi kwa kuongeza uwezo wetu wa kutekeleza mikakati ya kutengeneza ajira sambamba na kuongeza uwezo wa uzalishaji hasa kwa vijana na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu.

**Mheshimiwa Spika,** Ukuaji endelevu wa uchumi unatakiwa uweze kutengeneza fursa za ajira, ambazo zitapelekea kupunguza umaskini na utegemezi kwa kuufanya ukuaji huo wa uchumi uwe shirikishi zaidi. Kutokuongezeka kwa fursa za ajira hususan kwa vijana kunapunguza kasi ya kupungua kwa umaskini. Vijana ndio injini na tanuri ya maendeleo ya nchi yoyote ile duniani kwani ndio nguvu kazi ya kutegemea na hawapaswi kuwa tegemezi na kuwachwa mkono.

**MWELEKEO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia TZS 1,845.7 bilioni ikiwa na vipaumbele vya kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato ya Serikali, ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kimkakati kwa lengo la kuimarisha uchumi na huduma za kijamii, kudhibiti matumizi ya Serikali na kuimarisha utawala bora. Kiwango hichi cha bajeti ni sawa na ongezeko la asilimia 16.9 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021 ya TZS 1,579.2 bilioni. Ongezeko hili la asilimia 16.9 linatokana na kuongezeka kwa bajeti ya kazi za maendeleo pamoja na kuongezwa kwa Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Bajeti ya Serikali Kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufikia malengo ya bajeti hii, Serikali inapaswa iendelee tena kwa nguvu na ufanisi wa hali ya juu kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kuimarisha nidhamu ya matumizi.

## MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono azma ya Serikali ya kuanza kutoza Kodi ya Majengo (Property Tax) katika mwaka wa fedha 2021/2022 licha ya kuwa sheria yake ipo muda mrefu, haijaanza kutekelezwa kwa ufasaha tokea Mwaka 2008 mwezi Disemba ilipopitishwa na kusainiwa. Aidha, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutoza kodi hiyo kwa kiwango cha TZS 10,000 kwa nyumba za kawaida na TZS 10,000 kwa nyumba za ghorofa kwa mwaka kwani viwango hivi ni nafuu sana sana ukilinganisha na viwango vinavyotozwa takriban na nchi zote za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali wakati wa kukusanywa kodi hiyo, izingatie matakwa ya kisheria zinazosimamia jambo hili na uanishwaji wazi wa maeneo yaliyotajwa kisheria kwani kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha kodi hiyo (Sheria ya Kodi ya Majengo Nam. 14 ya mwaka 2008 pamoja na Marekebisho yake ya mwaka 2020) kuna aina kumi tatu (13) za majengo hayapaswi kutozwa kodi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanya haraka kwa kuihabarisha jamii kupitia vyombo vya habari na magazeti juu wa uwamuzi huu mwema wa Serikali ikiwemo aina ya majengo na kiwango cha kodi kinacholazimika kulipwa kwa lengo la kupokea maeneo yao kama kif 7 (3) &(4) kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa ni muda mrefu kodi hii imekuwa ikishindikana kukusanywa, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati maalumu kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha 2021/2022 kodi hii inaenda kukusanywa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali inakusudia kuleta mapendekezo ya kutokupandisha kodi yoyote, badala yake inapendekezwa kuendeleza jitihada za kuimarisha ulipaji na ukusanyaji wa mapato ya ndani kutokana na vyanzo vilivyopo, kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato. Kamati inaafikiana na Serikali juu ya hatua hizi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato bila ya kupandisha kodi yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua hizi ni bora zaidi kwani husaidia kuongeza mapato bila kudumaza uchumi kwa kuwaongezea mzigo wafanyabiashara na pia huleta ufanisi zaidi katika ukusanyaji wa mapato sambamba na kuimarisha udhibiti wa uvujaji wa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo litasaidia kuongeza mapato ni kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma na kuendelea kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya matumizi, hususan katika miradi ya maendeleo. Lengo hapa ni kupata thamani halisi ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Umakini katika kupanga matumizi na nidhamu ya usimamizi wa fedha za umma ndizo nguzo kuu za ufanisi wa utekelezaji wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mifumo ya kielekroniki pekee ndio itumike katika ukusanyaji wa mapato sambamba na kuharakisha taratibu za kuiunganisha mifumo yote hiyo katika mfumo mmoja mkuu ili mapato yote katika Wizara, Serikali za Mitaa na Taasisi zote za Umma

yakusanywe kwa uwazi na kwa ufanisi. Mifumo hii itasaidia kupunguza gharama za ukusanyaji kodi, upatikanaji wa taarifa sahihi za walipa kodi na ukadiriaji sahihi wa makusanyo ya mapato kwa taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la mwisho katika mambo ambayo Kamati inashauri ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ni kutafuta utatuzi wa haraka wa mkwamo wa usafirishaji wa bidhaa kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kuwajengea mazingira wezeshi wafanyabiashara wetu ili walipe kodi kwa hiyari na kuimarisha miundombinu yote shirikishi iwe ya ujenzi wa viwanda au uvunaji wa rasilimali mazao ya baharini na nchi kavu itakayopelekea kuongezeka kwa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi. Aidha, Serikali inapaswa kuendelea kuimarisha mazingira wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara yatakayomnufaisha muwekezaji na mzawa.

## SHUKURANI

**Mheshimiwa Spika**, Wapwani wanamsemo wao unaosema **'mwenda tenzi na omo marejeo ngamani'** kwa muktadha huu natoa shukurani zangu za dhati kwa Wananchi wezangu wa Jimbo la Pangawe na Kijitoupele  kwa kuendelea kuniamini na kunivumulia kwa kipindi chote hichi cha vikao vya bajeti, naamini niliwawakilisha na kuwasemea vyema.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia napenda kukushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 – 2023/2024 na pia kwa miongozo yako ambayo umekuwa ukitupatia. Aidha, kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunistahamilia na kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha hotuba hii. Mwisho, nawaomba Wajumbe waichangie na kuishauri Serikali ili bajeti hii ya kimkakati iwe bora na yenye tija kwa wananchi na hatimae waipitishe ili Serikali ikaitekeleze.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Ahsante

…………………

Mhe. Ali Suleiman Ameir,

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**